**SEHEMU YA A: USHAIRI**

**SWALI LA LAZIMA**

**Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo**

**MKULIMA**

Mtazameni …nguzo ya Afrika Mtumwa
wa watumwa waloridhiya!

Amekita jembe lake akilisujudia
Kwa tambo lililoumbuka na kuselehea
Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia
Na machungu ya maonevu alovumilia

Moyo wake nzito ulikomaa kama kuni
Haujui tena kutarajia wala kutamani
Umekufa ganzi, kutoishi wala huzuni

Basi iteni fikira mambo mukiyafikiri
*Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari*
Siku ukweli na hali yake utapodhihiri
Umejiandalilia vipi….

huo mkono ulomuumbua na kumkausha hizo
pumzi zilizomzimia taa ya maisha humfunga
kizuizini, gizani *kumtowesha?*

Ni jawabu gani aliowekewa na wakati
Kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti
Kuliwaza hamaki ya njaa hii ya dhati
Njaa ya maisha itakayo kushibishwa

**Maswali**

(a) Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika shairi hili (al.4)

(b) Taja na utoe mifano za aina zozote **mbili** za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi hili (al.4)

(c) Eleza umbo la shairi hili (al.2)

(d) Onyesha umuhimu wa matumizi ya kihisishi katika shairi (al.2)

(e) Fafanua maana ya:

(i) Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari (al,2)

(ii) Kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti (al.2)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi (al.3)

(i) tambo

(ii) ulokomaa

(iii) kumtoweka

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

**KIDAGAA KIMEMWOZEA: Ken Walibora**

2. Uzembe na mapuuza huathiri maendelo ya nchi. Thibitisha (al.20)

3. Ninyi ni ndugu? Naona mna mshabaha…….

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili? (al.4)

(ii) Mzungumzaji alikuwa mhusika wa sifa kandamizi. Eleza (al.10)

(iii) Wanaozungumziwa walikumbana na dhiki nyingi maishani mwao. Eleza kwa kutoa

mifano (al.6)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

**MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE**

4. Jina si kitu. Tumbo ndilo muhimu. Tumbo lako na jamaa yako

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)

(b) Fafanua jinsi tumbo limewekwa mbele ya jina katika tamthilia hii (al. 16)

5. Ufisadi unaendelezwa na Baraza. Eleza (al.20)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

**DAMU NYEUSI: (KEN WALIBORA NA SAIDI A. MOHAMMED)**

6. Ni matatizo gani yanayowakumba vijana wanaoenda masomoni ughaibuni

Fafanua kwa kurejelea hadithi ya ***Damu Nyeusi*** (al.20)

**SEHEMU YA E**

7. **FASIHI SIMULIZI**

(a) Eleza umuhimu wa aina zifuatazo za ngano katika jamii

(i) Ngano za mtanziko (al.6)

(ii) Fafanua umuhimu wa maigizo ya watoto (al.6)

(iii) Fafanua sifa **tano** za RARA (al.5)

(iv) Eleza dhima ya misimu kama kipera cha usemi